

# Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

## Wizara ya Fedha

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA)



## TAARIFA KWA UMMA

### **KUTEULIWA KWA BW. FRANK FRED SHANGALI KUWA MENEJA WA USIMAMIZI (STATUTORY MANAGER) WA KAMPUNI YA BIMA YA INSURANCE GROUP OF TANZANIA (IGT)**

**Dar es Salaam, 19 Julai, 2024**

Kamishna wa Bima Tanzania, Dkt. Baghayo Saqware, amemteua Bw. Frank Fred Shangali wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kuwa Meneja Usimamizi wa Kampuni ya Bima ya Insurance Group of Tanzania (IGT), kuanzia tarehe 19 Julai, 2024. Uteuzi huo ni kwa mujibu wa Kifungu cha 165 (1) (iv) cha Sheria ya Bima Sura 394 ambacho kinampa Mamlaka Kamishna kuteua Meneja wa muda ambaye atakuwa msimamizi wa Kampuni ili kuimarisha utendaji wa Kampuni husika.

Uteuzi wa Bw. Shangali ni moja ya hatua ambazo Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA) imechukua ili kuboresha shughuli za kiutendaji za kampuni ya IGT na kwamba mabadiliko hayo pamoja na mengine yanalenga kuimarisha utendaji wa Kampuni ili iweze kuendelea kutoa huduma bora za kibima kwa wananchi kama inavyotarajiwa na Mamlaka kwa mujibu wa Sheria ya Bima.

TIRA itaendelea kuwa bega kwa bega na kampuni za Bima nchini ili kuhakikisha soko la bima linaendelea kuwa salama, himilivu, lenye weledi na wakati wote itaendelea kulinda na kusimamia haki za Mteja wa Bima.

Imetolewa na;

Hadjia I. Maulid  
Meneja Uhustiano na Mawasiliano kwa Umma  
TIRA

✉ coi@tira.go.tz

🌐 www.tira.go.tz

📞 +255 222 132 537

📠 FB, IG, X: //@tira\_tz

Wasiliana nasi

Dodoma:  
+255 26 2321180

Dar es Salaam:  
+255(022)2132537

Zanzibar:  
+255 26 2321180

#TIRAkwaSokoSalamaLaBima